HATI YA MAKUBALIANO YA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA UHAMASISHAJI WA UWAZI KATIKA MAPATO YA MADINI, GESI ASILIA NA MAFUTA NCHINI TANZANIA

Kijarida cha Kukuza Uelewa

Kimeandaliwa na:

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu
[LHRC]
Jengo la Jaji Lugakingira
Kijitonyama – Dar es Salaam
S. L. P. 75254
Simu: +255 22 2773038/48 Nukushi: +255 22 2773037
Barua Pepe: lhrc@humanrights.or.tz
Tovuti: www.humanrights.or.tz

Yaliyomo

Utambulisho wa Kituo

Utangulizi

1.0 Uanzishaji wa mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta nchini Tanzania

2.0 Malengo ya mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta nchini Tanzania (TEITI)

3.0 Utawala/Usimamizi wa mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta nchini Tanzania (TEITI)

4.0 Kazi za Kikosi kazi cha mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta nchini Tanzania

5.0 Muundo wa Kikosi Kazi

6.0 Mikutano

7.0 Utoaji Taarifa wa Mpango wa Uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta (TEITI)

8.0 Uendelevu

9.0 Hitimisho

UTAMBULISHO WA KITUO

Tangu kuanzishwa kwake mwaka 1995, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, kimekua kwa kasi sambamba na maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini. Kituo hiki kinafanya kazi nchi nzima kupitia mipango yake ya huduma za mafunzo kwa jamii na ufuatiliaji wa ukiukwaji wa haki za binadamu. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina ushawishi wa mabadiliko ya sera, sheria na taratibu mbalimbali katika ngazi ya kitaifa kwa kupata nguvu na uhalali wa kuyatenda hayo kutoka kwa jamii.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimesajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Makampuni, sura ya 212 ya sheria za Tanzania kama shirika lisilo la serikali, la kujitolea na lisilo jitafutia faida kwa nia ya kugawana.

Shirika hili liliundwa kutokana na mradi wa haki za binadamu wa Shirika la Mpango wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania [TANLET].
Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina makao yake makuu jijini Dar es Salaam na ofisi ndogo mkoani Arusha.

Maono

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye HAKI na USAWA.

Tamko la Lengo Mahsusi

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali, lisilo la kutafuta faida kwa nia ya kugawana, lisilo na fungamano na chama chochote cha siasa, linalojibidisha kujenga uwezo wa jamii, kulinda, kutetea na kupigania haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

Maadili ya Shirika

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinaamini katika maadili ambayo hutoa mwongozo wa jinsi wanachama wake, bodi ya wakurugenzi, wafanyakazi na wadau wengine wanavyopaswa kuenenda. Maadili hayo ni kama yafuatayo:

- Uadilifu;
- Usawa;
- Uwazi;
- Uwajibikaji;
- Weledi; na
- Kujitoa na Kujitolea.

HATI hii ya Makubaliano ni kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ("Serikali"), Jumuiya ya Asasi za Kiraia za Tanzania ("Asasi za Kiraia") na Makampuni ya Uchimbaji madini, gesi asilia na mafuta ("Makampuni") ambayo yanafanya kazi nchini Tanzania kupitia wawakilishi wao halali na imesainiwa tarehe 10 Machi, 2010 katika jiji la Dar es Salaam, Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

Utangulizi

Kwamba, Serikali ya Tanzania ilijiunga na mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na Mafuta (Extractive Industries Transparency Initiative (EITI)) mwezi wa Februari, mwaka 2009, kwa kuahidi kati ya mambo mengine kuchapisha malipo yanayolipwa Serikalini na makampuni pamoja na kodi zinazopokelewa Serikalini kutoka kwa makampuni kulingana na vigezo na misingi ya mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi aslilia na mafuta(EITI); na

Kwamba, vigezo na misingi ya mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na Mafuta (EITI) unahitaji mpango wa kuweza kuangaliwa na wadau mbali mbali (MSG) wakiwemo wawakilishi wa Asasi za kiraia, Makampuni na Serikali; na

Kwamba, ni muhimu kutafsiri upeo na mpangilio wa mpango wa utekelezaji wa mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta Tanzania (Tanzania Extractive Industries Transparency initiative(TEITI);

Kwa hiyo, Serikali pamoja na Makampuni na Asasi za Kiraia wanakubaliana yafuatayo:

1.0 Uanzishaji wa mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta nchini Tanzania

1.1 Wahusika katika hati hii wanakubaliana na maamuzi chanya ya Serikali ya kujiunga na mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta, na pia wanaidhinisha kanuni na vigezo vya mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta(EITI);

1.2 Wahusika pia wanakubaliana kuanzisha na wanaanzisha mkakati wa Uhamasishaji wa Uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta nchini Tanzania(TEITI) kwa madhumuni ya kutekeleza misingi na vigezo vya mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta(EITI).

2.0 Malengo ya mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta

nchini Tanzania (TEITI)

2.1 Malengo ya mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta nchini Tanzania (TEITI) yatakuwa ni kuwezesha utoaji wa taarifa kwa uwazi na kwa mara kwa mara, kuhakiki (na ukaguzi wa hesabu iwapo itakuwa muhimu kufanya hivyo chini ya kanuni za mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta(EITI)) na uchapishaji wa malipo yaliyolipwa na makampuni Serikalini **("Malipo") .**

Kuhusianisha mapato yaliyopokelewa na Serikali kutoka kwenye Mapato ya madini, gesi asilia na mafuta **("mapato").**

2.2. Katika kutimiza malengo yake, mkakati wa uhama sishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi a silia na mafuta nchini Tanzania (TEITI), Utahakiki sha:

Utoaji taarifa kwa uwazi na uchapishaji(usambazaji) taarifa kwa njia mbali mbali na kwa kuzingatia kanuni za mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta (i) malipo yaliyolipwa na makampuni kwa mawakala wote na idara zote za serikali; na (ii) Kuhusianisha mapato yaliyopokelewa na mawakala na idara zote za Serikali kutoka kwa makampuni.

Kwamba, shughuli zote za mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta (EITI), mchakato na mahitaji yatatumika kwa usawa au yatahusisha makampuni yote yanayofanya kazi Tanzania ikijumuisha Makampuni yote yanayomilikiwa na Serikali na mawakala kama vile Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na Shirika la maendeleo ya petroli Tanzania (TPDC) pamoja na mawakala wengine ambao serikali ni wadau; na

Kwamba muundo, utekelezaji, tathmini na mabadiliko ya shughuli za mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta(EITI) na mchakato mzima utafanyika kwa ushirikiano wa Asasi za Kiraia, Makampuni na Serikali watakaofanya kazi kwa pamoja kama wadau.

3.0 Utawala/Usimamizi wa mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta nchini Tanzania (TEITI)

Mahusiano ya mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta nchini Tanzania (TEITI) pamoja na utekelezaji wa shughuli na mipango yote vitasimamiwa na/au vitakuwa chini ya usimamizi wa wadau wa Kikosi

kazi (“Kikosi kazi”) cha mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta nchini Tanzania, ambacho ni chombo cha uangalizi kinachojumuisha wawakilishi wa wadau wa hati hii ya makubaliano. Hadidu rejea (TOR) ya kikundi imetolewa katika kipengele namba 4.0 kama ifuatayo.

4.0 Kazi za Kikosi kazi cha mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta nchini Tanzania

Kikosi kazi cha mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta nchini Tanzania (TEITI) ndicho kitakachokuwa kikundi cha utawala au uongozi wa mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta nchini Tanzania(TEITI). Kitakuwa na majukumu na mamlaka yafuatayo:

Kuandaa na/au kuidhinisha mpango kazi wa mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta nchini Tanzania (TEITI);

Kuandaa na kuidhinisha bajeti ya mkakati wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta nchini Tanzania (TEITI), na kuangalia utekelezaji wake;

Kuruhusu na/au Kuidhinisha vyanzo vya mapato.

Kuajiri na/au kuidhinisha uteuzi wa wakuu na wafanya-

kazi wengine waandamizi wa sekretarieti pamoja na kufuatilia na kutathmini utendaji wao;

Kuajiri afisa tawala huru;

Kupitisha au kuidhinisha utafutaji wa washauri au wataalamu wote na masomo;

Kupitisha na kuidhinisha machapisho ya ripoti za TEITI;

Kuendeleza na/au kuidhinisha sera muhimu za TEITI zinazohusiana na fedha na manunuzi na sera nyingine zote pamoja na taratibu zinazohitajika kwa ajili ya ufanisi na usimamizi wa uwazi wa TEITI;

Kuanzisha Kamati zinazohitajika na kukasimisha mamlaka yake yoyote kwa kamati hizo;

Kudumisha uhusiano wa karibu na sekreterieti ya EITI ya kimataifa, nchi nyingine tekelezi, na ya Washirika wa Maendeleo kikazi,

Kupitisha kanuni kadri zitakavyohitajika kwa ajili ya utawala wa ndani na kwa ajili ya utendaji wa sekretarieti; na

Kuchukua hatua na kufanya kazi zitakazohitajika ili kufikia malengo ya TEITI.

5.0 Muundo wa Kikosi Kazi

5.1 Kikosi kazi kitakuwa na wajumbe wafuatao:

Mwenyekiti wa wadau wa Mpango wa Uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta.

Wajumbe 5 wawakilishi wa serikali;
Wajumbe 5 wawakilishi wa makampuni; na
Wajumbe 5 wawakilishi wa asasi za Kiraia

5.2 Wajumbe wa Kikosi kazi watateuliwa kwa kipindi cha miaka mitatu ukiwepo uwezekano wa kuteuliwa tena kwa kipindi kingine.

6.0 Mikutano

6.1 Akidi ya kikosi kazi katika mikutano itakuwa ni kwa wingi wa nusu ya idadi ya wajumbe wote , ambayo ita jumuisha angalau mwakilishi mmoja kutoka kwa kila mdau (yaani Serikali, Makampuni, Asasi za Kiraia);

6.2 Kikosi kazi kitaamua mambo yote kwa makubaliano.

6.3 Kikosi kazi kitakutana angalau mara moja kwa mwezi mpaka zoezi la kwanza la uthibitisho litakapokamilika.

Wingi wa mikutano unaweza rejewa na kikosi kazi baada ya uthibitisho.

7.0 Utoaji Taarifa wa Mpango wa Uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na ma futa (TEITI)

7.1 Mpango wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta(TEITI) utatangaza kila mwaka kwa kuzingatia misingi mbalimbali, taarifa (taarifa ya mpango wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta-TEITI) ikiwa na:

Malipo yaliyofanywa na makampuni kwa serikali na;

Mapato husika yaliyokusanywa na serikali (ikiwa ni pamoja na serikali za mitaa) kutoka katika makampuni.

7.2 Kikosi kazi kitaanzisha au kusababisha uanzishwaji wa namna muhimu ya kutoa taarifa (kiolezo) ambacho ki tatumwa kwa wadau wote wa serikali na makampuni (watoa taarifa) pamoja na maelekezo ya namna ya ku jaza kiolezo hicho, na lini na wapi kiolezo hicho ki wawasilishwe baada ya kujazwa.

7.3 Kikosi kazi kitateua au kuajiri msimamizi huru ambaye atachambua, atakagua,kukusanya na/au kupitia mawasilisho ya serikali na makampuni kwa ajili ya uandaaji wa taarifa ya mpango wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta (TEITI).

Msimamizi atawasilisha taarifa kwa Kikosi kazi kwa mujibu wa mkataba wa Msimamizi na taratibu zenye usiri na uaminifu.

7.4 Kikosi kazi kitachapisha au kuidhinisha machapisho ya ripoti ya mpango wa uhamasishaji wa uwazi katika ma pato ya madini, gesi asilia na mafuta(TEITI), ikiwa ni pamoja na maoni ya msimamizi.

8.0 Uendelevu

8.1 Wadau watakaoshirikishwa katika Mpango wa uhamas ishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta (TEITI) watafuatilia au kuchukua hatua za kish eria na za kiutawala itakapobidi au kuhitajika ili ku hakikisha kwamba;

Malengo ya mpango wa uhamasishaji wa uwazi katika ma-pato ya madini, gesi asilia na mafuta(TEITI) yanafikiwa ki-kamilifu na matokeo yanasambazwa.

Kwamba mpango wa uhamasishaji wa uwazi katika ma-pato ya madini, gesi na mafuta (TEITI) unaungwa mkono na kufadhiliwa kwa namna endelevu.

Kwamba kila shughuli au mpango utakaofanywa ili kuendeleza mpango wa uhamasishaji wa uwazi katika ma-

pato ya madini, gesi na mafuta(TEITI) umeruhusiwa kisheria na kutekelezeka.

8.2 Kwa kutambua changamoto zinazoweza kujitokeza katika utekelezaji wa malengo ya mpango wa uhama sishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta(TEITI), wadau wanafahamu faida za mpango huu, na wamelenga kufanya kazi kwa pamoja ili kudhibiti kero, kutatua tofauti na kuendelea kutekeleza malengo ya mpango wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi asilia na mafuta(TEITI) katika nyanja ya utatu (Serikali, Makampuni na Asasi za kiraia).

9.0 Hitimisho

9.1 Hati hii ya makubaliano inahusisha kauli ya msingi ya uanzishwaji wa malengo ya mpango wa uhamasishaji wa uwazi katika mapato ya madini, gesi na mafuta (TEITI) pamoja na utekelezaji wake.

9.2 Hati hii ya makubaliano inaweza kufanyiwa mareke bisho na theluthi mbili (2/3) ya wajumbe wote wa kikosi kazi kuzingatia kigezo kwamba wajumbe wote wa kikosi kazi wanaopigia kura marekebisho hayo ya makubaliano watakuwa na angalau mwakilishi mmoja kutoka katika kila kundi la wadau.

<u>Wasiliana nasi:</u>

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu
Legal and Human Rights Centre [LHRC]
S. L. P. 75254, Dar es Salaam - Tanzania
Simu: +255 22 2773038/48; Nukushi: +255 22 2773037
Barua Pepe: lhrc@humanrights.or.tz
Tovuti: www.humanrights.or.tz

Ofisi ya Arusha
Barabara ya Engira, Kitalu Na. 48
S. L. P. 15243 - Arusha
Simu: +255 27 2544187
Barua Pepe: lhrcarusha@humanrights.or.tz

Kituo cha Msaada wa Sheria
Mtaa wa Isere - Kinondoni
S. L. P. 79633 - Dar es Salaam
Simu/Nukushi: +255 22 2761205/6
Barua Pepe: legalaid@humanrights.or.tz